



MWALIKO KWA WENYE NIA YA KUNUNUA HISA NA KUWEKEZA MTAJI KWENYE BENKI YA TWIGA

Kwa mamlaka iliyopewa kisheria kupitia kifungu namba 56(1) (g) (i) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania ilichukua usimamizi wa benki ya Twiga Bancorp Ltd (Twiga) kuanzia tarehe 28 Oktoba, 2016.

Hatua hii ilichukuliwa baada ya kubainika kuwa benki ya Twiga ilikuwa na upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na vigezo vilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya 2006 na kanuni zake. Aidha, kuendelea kufanya biashara katika hali hii kungehatarisha uthabiti wa sekta ya fedha, maslahi ya wenye amana na wadai wengine.

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 58(2)(i) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeamua kutatua tatizo la upungufu wa mtaji kwa kuwakaribisha wenye nia ya kununua hisa na kuleta mtaji kwenye benki hii. Kwa kuzingatia kifungu cha 59(6) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya 2006, Benki Kuu ya Tanzania inawaalika watu binafsi na makampuni ya ndani na nje ya nchi wenye nia ya kununua hisa na kuleta mtaji mpya kwenye benki ya Twiga, kuwasilisha maombi yao Benki Kuu ya Tanzania.

Maombi hayo yawasilishwe kwa Gavana, Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam. Maombi yawasilishwe kwa maandishi yakiwa yameandikwa “**Mwaliko kwa Wenye Nia ya Kununua Hisa na Kuwekeza Mtaji Kwenye Benki ya Twiga**”. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa, tarehe 11 Novemba 2016 kabla ya saa 10.30 jioni. Watakaotimiza vigezo wataalikwa kufanya upembuzi wa hali ya kifedha ya benki ya Twiga hadi kufikia Ijumaa tarehe 18 Novemba 2016 ili kutoa nafasi kwa hatua zingine kuendelea. Utoaji wa taarifa za mahesabu kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa hali ya fedha ya Twiga utafanyika baada ya kusaini Makubaliano ya Kuhifadhi Siri (Confidentiality Agreement).

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mabenki kwa simu namba +255 22 2235483, nukushi +255 22 2234189 au barua pepe kanyoni@bot.go.tz.

BENKI KUU YA TANZANIA

8 NOVEMBA 2016